AFRICAN UNION
الاتحاد الأفريقي
UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE
UNIÃO AFRICANA
UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844
Website: www.au.int

BARAZA LA UTENDAJI
Kikao cha Kawaida cha Arobaini na Nne
Tarehe 15 Januari - 15 Februari 2024
Addis Ababa, ETHIOPIA

EX.CL/1462(XLIV)
Matini Chanzi: Kiingereza

RIPOTI YA KAMATI NDOGO KUHUSU MAKAO MAKUU NA MIKATABA YA UENYEJI

I. UTANGULIZI

1. Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Makao Makuu na Mikataba ya Uenyeji ilifanya mkutano tarehe 5 Desemba 2023 kwa njia ya Mtandao, kujadili jedwali la masuala yaliyosalia yanayohusu utekelezaji wa Makao Makuu na Mikataba ya Nchi Mwenyeji.

2. Mkutano uliongozwa na Mhe. Dkt. Mohamed Omar Gad, Balozi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri nchini Ethiopia na Mwakilishi wa Kudumu kwenye Umoja wa Afrika, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Makao Makuu na Mikataba ya Uenyeji.

II. MAHUDHURIO

3. Wajumbe wafuatao wa Kamati Ndogo walihudhuria:

    1. Misri (Mwenyekiti)
    2. Ethiopia
    3. Chad
    4. Namibia
    5. Msumbiji
    6. Afrika Kusini
    7. Senegal
    8. Gambia
    9. Tanzania

III. HOTUBA YA UFUNGUZI

4. Katika hotuba yake ya ufunguzi, Mhe.Balozi Mohamed Gad aliwakaribisha wajumbe na kuishukuru Sekretarieti (OLC) kwa kuwezesha kuandaliwa kwa mkutano.

5. Balozi huyo alisisitiza zaidi kazi muhimu inayofanywa na Kamati Ndogo, na kuthibitisha tena ahadi ya Misri ya kutekeleza kazi ya Kamati Ndogo na kuhakikisha utendaji sahihi na mzuri wa AU na Vyombo vyake kuhusiana na masuala yaliyo ndani ya mamlaka ya Kamati Ndogo.

6. Kutokana na ukweli kuwa Kamati ndogo haina Hadidu za Rejea (ToRs) kudhibiti na kuongoza kazi yake, hivyo balozi aliiomba Sekretarieti kuandaa rasimu ya Hadidu za Rejea kwa ajili ya Kamati ndogo itakayowasilishwa na kujadiliwa baada ya Mkutano Mkuu wa Februari.

7. Kwa kurejelea kwenye nyaraka zilizosalia zitakazojadiliwa kwa pamoja na Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Kanuni, Viwango na Sifa (inayoongozwa na Zimbabwe), yaani (*Draft Model Host Agreement for AU Institutions/ Draft Model Host Agreement for AU Meetings/ Revision of the Criteria for Hosting AU Organs, Institutions and Specialized Agencies*), Mhe. Balozi Mohamed Gad alipendekeza kuwa kujadiliwa kwa nyaraka hizi za kisheria kufanyike

baada ya Februari 2024 kwa kuzingatia ratiba iliyobana ya Nchi Wanachama zinazojiandaa na Mkutano Mkuu Ujao.

8. Balozi huyo alihitimisha hotuba yake ya ufunguzi kwa kusisitiza kuwa Kamati Ndogo inakosa Wajumbe Wawili (2), mmoja kutoka Kaskazini na mwingine kutoka Ukanda wa Magharibi, kwahiyo aliiomba Sekretarieti kuwasiliana ipasavyo na Wakuu husika wa kanda hizo kuchagua Mjumbe mmoja kutoka Kaskazini na kumbadilisha Mjumbe aliyesimamishwa kutoka Magharibi, kama ilivyo desturi.

IV. KUJADILI NA KUPITISHA AJENDA

9. Vipengele vifuatavyo vya ajenda vilijadiliwa wakati wa Mikutano miwili ya Kamati Ndogo:

   a. Hotuba ya Ufunguzi – Mwenyekiti
   b. Kujadili na kupitisha rasimu ya ajenda
   c. Kujadili Jedwali la Masuala yaliyosalia
   d. Mengineyo
   e. Hotuba ya ufunguzi – Mwenyekiti

V. TAARIFA JUU YA HALI YA UTEKELEZAJI YA JEDWALI LA MASUALA YALIYOSALIA:

10. Ofisi ya Mshauri wa Sheria iliwasilisha jedwali la masuala yaliyosalia na Mwenyekiti anayeongoza alifungua majadiliano. Wajumbe waliohudhuria waliipongeza Sekretarieti kwa toleo lililosasishwa la jedwali la masuala yaliyosalia yanayohusiana na mamlaka ya Kamati Ndogo.

11. Mkutano uliomba Sekretarieti kusasisha orodha ya barua pepe za wajumbe wa Kamati Ndogo ili kuwezesha upelekaji sahihi wa nyaraka za mikutano au mawasiliano mengine yoyote yale yanayohusiana na mamlaka ya kamati ndogo.

12. Mkutano ulizingatia zaidi kuwa baadhi ya vipengele kwenye jedwali vinahitaji kubadilishwa tena na kusahihishwa ili kuepuka urudiaji wowote na kurekebisha lugha ili kuifanya iwe sahihi zaidi na ya kidiplomasia.

13. Mkutano uliomba Sekretarieti kutoa taarifa ya mara kwa mara na kwamba vipengele vyote viwasilishwe kwa wasimamizi ndani ya OLC.

14. Jamhuri ya Kiarabu ya Misri iliipongeza Sekretarieti kwa taarifa iliyotolewa kwa mkutano na uandaaji wa mkutano wa kiufundi na idara husika kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Misri mnamo tarehe 27 Novemba 2023, ambao ulilenga kwenye kurekebisha na kuoanisha lugha ya nyaraka.

15. Baada ya hapo, Mwakilishi Mashuhuri wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri aliiomba Sekretarieti kuhitimisha na kugawa toleo safi lililosasishwa ili kuitisha mkutano wa mwisho wa kuhitimisha, lengo likiwa kuwa mkataba utakuwa tayari kusainiwa pembezoni mwa Mkutano Mkuu wa Februari 2024.

16. Mjumbe mashuhuri kutoka Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alieleza wasiwasi wake kuwa jedwali lilihitaji kusasishwa. Alisisitiza kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan kuhusu Makao Makuu ya! Umoja wa Posta wa Afrika (PAPU) imefanya mambo zaidi lakini maendeleo hayo mapya hayamo kwenye jedwali linalojadiliwa. Hivyo, alikubali kuwasilisha rasmi kwa Sekretarieti ya Kamati ndogo maendeleo yote mapya na vifaa ambavyo vimetolewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili jedwali lisasishwe ipasavyo.

17. Mjumbe Mashuhuri kutoka Jamhuri ya Afrika Kusini aliutaarifu mkutano kuwa kuna mashauriano yanayoendelea kuhusu suala la Mikataba ya Nchi Mwenyeji ya Taasisi za AU ambazo mwenyeii wake ni Afrika Kusini kwa kuzingatia Sheria za ndani. Aliutaarifu zaidi mkutano kuwa pendekezo la kusimamia ofisi zote za AU ambazo mwenyeji wake ni Afrika Kusini katika Eneo moja pia lipo katika majadiliano.

18. Kuhusiana na suala la Nchi Wanachama ambazo zilinyimwa viza kushiriki mkutano ulioandaliwa na taasisi za AU nchini Afrika Kusini, iliombwa kuwa taarifa za kina zitolewe kwa Serikali ya Afrika Kusini ili suala hilo liweze kushughulikiwa kwa wakati na mamlaka husika.

19. Mwakilishi Mashuhuri wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia alielezea wasiwasi wake kuhusiana na mtiririko wa taarifa akisema kuwa hakupokea ujumbe kuhusu mkutano huu. Aliiomba Sekretarieti kusasisha orodha ya barua pepe kama ilivyokuwa imependekezwa na wajumbe wengine. Alitoa zaidi taarifa kwa mkutano kuwa baadhi ya hatua zimechukuliwa kushughulikia baadhi ya masuala yaliyosalia. Alisema kuwa leseni za udereva kwa sasa zinatolewa kwa kugha ya Kiingereza na kiamhari. Zaidi ya hayo, aliutaarifu mkutano kuwa kiwango cha Dola za Marekani ambazo zinawezwa kubebwa na kuingia nchini Ethiopia kimeongezwa kutoka Dola 3000 hadi Dola 10,000. Zaidi, kuhusu suala la fedha na vitu vingine vya thamani vilivyoshikiliwa, aliutaarifu mkutano kuwa uamuzi wa kisiasa wa kipekee wa kurudisha fedha zilizoshikiliwa kwa wahusika umechukuliwa na kuna maendeleo katika suala hili. Kuhusiana na masuala mengine yaliyosalia, Mwakilishi Mashuhuri alielezea ahadi ya nchi mwenyeji ya kuendelea kufanya kazi kwa kushirikiana kwa karibu na Tume ya Umoja wa Afrika na wadau wengine kutatua masuala yote yaliyosalia.

VI. HITIMISHO :

20. Mwenyekiti alitoa hitimisho na mapendekezo yafuatayo:

(i) Alizingatia wasilisho lililotolewa na OLC juu ya Jedwali la masuala yaliyosalia, na la maoni na mitazamo yaliyotolewa na Wajumbe wa Kamati Ndogo, pamoja na majibu yaliyotolewa na Tume juu yake;

(ii) Alizipongeza Nchi Wanachama na Tume kwa maendeleo yaliyofikiwa kwenye kutatua masuala yaliyosalia yanayoathiri shughuli za Umoja wa

Afrika katika nchi zao, na kuiomba OLC kuendelea kusasisha Jedwali la masuala yaliyosalia na kumpa kazi msimamizi wa kitaifa ndani ya OLC kwa ajili ya kazi hii;

(iii) Aliiomba Tume kusasisha taarifa iliyopo, ikiwa ni pamoja na kufichua hali zozote zinazorejelewa kwenye jedwali kwa ajili ya kuwa na uwazi na hatua ya Nchi Wanachama;

(iv) Alielekeza kuwa OLC iandae rasimu ya Hadidu za rejea kwa ajili ya Kamati ndogo itakayowasilishwa kwa Kamati ndogo mwezi Aprili 2024 kwa ajili ya kujadiliwa;

(v) Aliiomba Sekretarieti kuwasiliana rasmi na Wakuu wa Kanda za Kaskazini na Magharibi kumaliza uundaji wa Kamati Ndogo;

(vi) Mwisho, mkutano uliomba kuwa Sekretarieti isasishe orodha ya barua pepe za Wanachama wa Kamati ndogo.

VII. MENGINEYO

21. Kwavile hakukuwa na mengineyo, Mwenyekiti wa Kamati ndogo aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria na kushiriki kwenye mkutano na alifunga mkutano.

RASIMU YA MAAMUZI JUU YA RIPOTI YA KAMATI NDOGO KUHUSU MAKAO MAKUU NA MIKATABA YA UENYEJI

Baraza Kuu,

1. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kamati Ndogo kuhusu Makao Makuu na LINAIOMBA Tume kuendelea na mashauriano na Nchi Wenyeji kushughulikia masuala yote yaliyosalia katika jedwali.

2. **LINAIOMBA** Tume kuandaa Hadidu za Rejea (ToRs) za Kamati Ndogo kuhusu Makao Makuu na Mkataba wa Nchi Mwenyeji kabla ya Aprili 2024 na kuziwasilisha kwa Kamati Ndogo kwa ajili ya kujadiliwa na kupelekwa mbele kwa PRC kwa ajili ya kupitishwa kwa mujibu wa Kanuni Zilizopo za Utaratibu za Umoja wa Afrika.

3. **LINAIOMBA** Sekretarieti na Nchi Wanachama ambazo ni wenyeji wa Vyombo, Taasisi na Ofisi za AU kutoa taarifa za mara kwa mara kwa Wajumbe wa Kamati Ndogo juu ya masuala mapya ambayo yanahitaji umakini wao.

4. **LINAPONGEZA** jitihada zilizofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na ahadi yake ya kukamilisha Mkataba wa Nchi Mwenyeji wa Ujumbe wa Kudumu wa Umoja wa Afrika kwenye Jumuiya ya Nchi za Kiarabu unaosimamiwa mjini Cairo, Misri.

5. **LINAPONGEZA** jitihada zinazofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia katika kushughulikia masuala yaliyosalia kwenye jedwali na **LINAPONGEZA** maboresho yanayoendelea ya utendaji kazi mzuri wa Tume ya Umoja wa Afrika na jumbe za kidiplomasia ambazo mwenyeji wake ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia.

6. **LINAIPONGEZA** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sekretarieti ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU) kwa kumaliza ujenzi na kuzindua Makao Makuu ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU) mjini Arusha, Tanzania.

7. **MWISHO LINAPONGEZA** ahadi ya Serikali ya Jamhuri ya Afrika Kusini kuhitimisha mashauriano yanayoendelea kuhusu Mikataba ya Nchi Mwenyeji na Taasisi za AU ambazo mwenyeji wake ni Afrika Kusini na **LINAIOMBA** Kamati Ndogo kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Afrika Kusini kukamilisha suala hili.

AFRICAN UNION UNION AFRICAINE

African Union Common Repository **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-01-15

Report of the PRC sub-committee on Headquarters and Host Agreements

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10499

Downloaded from African Union Common Repository